

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS –TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA ULANGA



Tarehe: 18/05/2020

TANGAZO LA ZABUNI
NAMBA YA ZABUNI LGA/082/2020-2021/HQ/NC/01 Lot 1 – 4/ 04
ZABUNI YA UKUSANYAJI USHURU MBALIMBALI WA VYANZO VYA MAPATO NA UZOAJI
TAKA NGUMU KWA MWAKA 2020/2021

Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga inakusudia kuweka wazabuni wa Utozaji Ushuru wa vyanzo mbalimbali vya mapato kwa mwaka 2020/2021.

Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga inapenda kuwaalika watu Binafsi, Makampuni, Ushirika, Taasisi au Vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria, wenye nia na uwezo wa kufanya kazi hizo, watume maombi yao kwa zabuni zifuatazo:-

NA.	AINA YA ZABUNI	NAMBA YA ZABUNI	ENEO LA KUKUSANYA USHURU
1.	Ushuru wa mazao ya chakula na nafaka	LGA/082/2020/2021/H Q/NC/01 - Lot 01	Eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga
2.	Ushuru wa Mazao ya Misitu i.e. Mbao, Mkaa, Nguzo, Mirunda, Magogo, Kuni na Mazao mengine ya misitu.	LGA/082/2020/2021/H Q/NC/01 - Lot 02	Eneo lote la Halmashauri ya Ulanga isipokuwa mazao ya kiwanda cha KVTC
3.	Ushuru wa Minada	LGA/082/2020/2021/H Q/NC/01 - Lot 03	Mnada wa Lukande, Iputi, Mavimba, Mbuyuni na Mbenja katika Halmshauri ya Wilaya ya Ulanga
4.	Ukusanyaji wa ushuru wa madini ya ujenzi i.e Mchanga, mawe, kokoto na kifusi.	LGA/082/2020/2021/H Q/NC/01 - Lot 04	Eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga
5.	Ukusanyaji ushuru wa taka, ukusanyaji wa taka ngumu na ubebaji kutoka Kata ya Mahenge mjini hadi Dampo la Mbagula	LGA/082/2020/2021/H Q/NC/04	Kata ya Mahenge Mjini

MASHARTI YA MAOMBI YA ZABUNI

Maombi yote ya zabuni yazingatie masharti yafuatayo:-

1. Nyaraka za zabuni zitapatikana baada ya kulipa ada ya kila zabuni husika. Ada hiyo haitarejeshwa (Non refundable). Mwombaji atalipa ada ya maombi ya Tshs. 150, 000/= kwa Zabuni Na. 1 – 4 na 60,000.00 kwa Zabuni Na. 5 fedha zilipwe kwenye akaunti Na. 21910000381 - NMB Ulanga baada ya kupata kifungu cha kulipia (Control number) kutoka Ofisi ya Mweka Hazina wa Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga.
2. Ombi la zabuni liwe na jina la zabuni anayoomba, aidha aonyeshe mahali ofisi yake ilipo.
3. Mwombaji atatakiwa kuambatanisha kivuli cha leseni ya biashara iliyo hai, kivuli cha usajili wa kampuni, usajili wa VAT/TIN na uwakilishi wa kisheria "Power of Attorney" pamoja na miamala ya benki (bank statement) ya miezi mitatu kabla ya tarehe ya tangazo hili, pia aambatanishe na wasifu wa Kampuni "Company Profile" ya kampuni hiyo.
4. Mwombaji atatakiwa kutoza viwango halali vilivyoidhinishwa na Sheria mama na Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga.
5. Iwapo mzabuni atachaguliwa, atatakiwa kuwasilisha dhamana ya utendaji "Performance guarantee" kutoka bank au Kampuni ya Bima inayokubalika na Mwajiri.
6. Mwombaji aorodheshe vifaa alivyonavyo, idadi ya wafanyakazi na uzoefu wao. Pia mwombaji aoneshe uzoefu alionao katika zabuni hiyo.
7. Mwombaji aandike juu ya bahasha na kwenye barua ya maombi, aina na namba ya zabuni anayoomba. Atatakiwa kutuma kabrasha halisi (original) na nakala (copy) mbili (2) na yawekwe kwenye bahasha moja. Juu ya bahasha kusiandikwe wala kuwekwa alama yoyote zaidi ya jina la zabuni, namba ya zabuni na anuani ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga.
8. Mwombaji atoe tamko la kutojikusisha na vitendo vya rushwa.
9. Halmashauri hailazimiki kukubali zabuni ya bei ya juu isipokuwa kwa vigezo muhimu vilivyopo katika tangazo hili na kabrasha la zabuni.
10. Maombi yafungwe kwenye bahasha ya khaki kwa lakiri na kutumwa kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni kwa anuani ifutavyo:-

Katibu wa Bodi ya Zabuni,
Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga,
S.L.P 22, Ulanga.

11. Kabrasha la zabuni linapatikana katika ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga.
12. Mwisho wa kupokea maombi hayo ni tarehe 01.06.2020 *saa nne (4) asubuhi*. Waombaji au wawakilishi wao, wanaalikwa kuhudhuria ufunguzi wa zabuni hizo utakaofanyika katika ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri. Aidha, unashauriwa kutembelea eneo la kazi ndani ya Wilaya ya Ulanga kabla ya kuleta maombi kwa gharama zake.



JONAS E. MALLOSA,
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
ULANGA

MKURUGENZI MTENDAJI (WY)
HALMASHAURI YA WILAYA
ULANGA